# HALI HALISI YA MAJADILIANO YA BIASHARA YA KIMATAIFA KWENYE MAENEO YA MAJADILIANO

## 1.0 Utangulizi

Tanzania ni nchi mwanachama wa Shirika la Biashara la Dunia (WTO) toka kuanzishwa kwa Shirika hilo mwaka 1995 ambapo makao makuu yake ni Geneva nchini Switzerland. Lengo mahususi la kuanzishwa kwa Shirika hilo ilikuwa ni kuhakikisha uwepo wa mtiririko mzuri wa Biashara (good trade flow) utakaochagiza maendeleo duniani kote hasa kwa nchi wanachama. Tangu kuanzishwa kwa Shirika hilo kumekuwapo duru nyingi za majadiliano, la kwanza likiwa ni la Singapore mwaka 1996 ambapo moja ya agenda zake ilikuwa ni Kurahisisha Biashara (trade facilitation), agenda hiyo na zingine kama vile uasili wa bidhaa (rules of origin), Masoko kwa Bidhaa Zisizokuwa za Kilimo (Non Agricultural Market Access), ushindani wa mauzo nje (export competition), serikali kununua na kuhifadhi chakula (Public Food Stockholding), na nyinginezo ziliingizwa katika duru la majadiliano huko Doha nchini Qatar mwaka 2001. Toka duru hilo Nchi Changa (LDCs) za WTO ikiwemo Tanzania zimeendelea kutetea misimamo yake ya kutaka kuendelea kumaliza majadiliano katika agenda za duru la Doha ambapo agenda zake nyingi zinatoa mwanya wa maslahi mapana kwa Nchi zilizo katika kundi la Nchi changa duniani (LDCs).

Hali halisi ya utekelezaji wa maamuzi ya Mawaziri wa Biashara kwenye maeneo mbalimbali ya WTO katika majadiliano yaliyofanyika Nairobi, Kenya mwaka 2015 ni kama ifuatavyo: -

### 1.1 Mkataba wa Kurahisisha Biashara *(Trade Facilitation Agreement)*

Kuhusu Mkataba wa Urahishaji Biashara, nchi wanachama wa WTO wamekamilisha majadiliano na uandaaji wa Itifaki ya marekebisho *(amendment protocol)* inayojumuisha Mkataba huo kuwa mmoja ya mikataba ya Shirika la Biashara la Dunia. Itifaki hiyo ilipitishwa na Baraza Kuu la Shirika la Biashara la Dunia *(WTO General Council)* mwezi Novemba, 2014. Baada ya taratibu zote kukamilika kuhusu Mkataba wa Urahisishaji Biashara, nchi wanachama zinatakiwa kuridhia kupitia Mabunge yao kwa ajili ya kuanza kutekelezwa rasmi. Kwa taratibu za WTO, Mkataba huo utaanza kutumika rasmi baada ya Itifaki ya marekebisho inayojumuisha Mkataba husika kuridhiwa na theluthi mbili (2/3) ya nchi wanachama wa WTO kulingana na Kifungu cha 3 cha Ibara ya 10 ya Mkataba wa WTO. Kutokana na taarifa za hadi tarehe 22 Januari, 2016 ni nchi 67 tu ndizo ambazo zimewasilisha WTO taarifa za kuridhiwa kwa Mkataba

huo kwenye nchi zao. Nchi zingine bado ziko kwenye hatua mbali mbali za kuridhiwa kwa Mkataba huo. Hata hivyo hakuna tarehe maalum iliyopangwa ya kupitishwa kwa mkataba huo ingawa kuna mashinikizo kutoka nchi tajiri kutaka mkataba huo uweze kuridhiwa mapema iwezekanavyo.

Sambamba na hili nchi wanachama zinatakiwa kuwasilisha WTO Sekretariati maeneo ya Kundi A *(Category A Measures)* ambayo yatakuwa sehemu ya Mkataba wa kurahisisha biashara ambayo utekelezaji wake utaanza mara moja punde Mkataba utakapoanza kutumika.

Tanzania kwa upande wake, ni moja ya nchi sabini na saba (77) ambazo hadi tarehe 7 Januari, 2016 tayari zimeshawasilisha WTO Sekretariati maeneo ya Kundi A ambayo itakuwa tayari kutekeleza pale Mkataba wa Kurahisha Biashara utakapoanza kutumika rasmi.

Suala ambalo bado halijakamilika kwa upande wa Tanzania ni kuridhiwa kwa Itifaki ya marekebisho *(amendment protocol)* inayojumuisha Mkataba huo wa kurahisisha biashara. Aidha, tayari rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri umeshaandaliwa na kilichobaki kwa sasa ni viambatisho hususani maoni ya wadau.

### 1.2 Serikali kununua na kuhifadhi chakula *(Public Stockholding for food Security)*

Kuhusu Serikali Kununua na Kuhifadhi Chakula *(Public Food Stockholding)*, mkutano wa Mawaziri uliofanyika mjini Bali mwaka 2013, iliamuliwa kuwa Serikali za nchi zinazoendelea ziruhusiwe kuendelea na utaratibu wao na programu za kununua chakula kutoka kwa wakulima na kuhifadhi kwa ajili ya usalama wa chakula kama suluhisho la muda mfupi wakati suluhisho la muda mrefu likitafutwa. Aidha, katika majadiliano, nchi zinazoendelea zikiongozwa na kundi la G33 ambalo Tanzania ni mjumbe zinataka suala hili liwe ni moja ya maeneo yatakayoruhusiwa bila masharti. Moja ya masharti yaliyowekwa katika mkataba wa Kilimo wa Shirika la Biashara ni ukomo wa kiasi cha fedha za Serikali (ruzuku) kwa ajili ya kununua chakula kutoka kwa wakulima wa nchi husika.

Ukomo huo ni kiasi cha asilimia 10 tu ya thamani ya uzalishaji wa nchi husika ambao unakokotolewa kutoka katika bei rejea ya mwaka 1986 na 1988. Kutokana na kupanda sana kwa bei za vyakula kwa miaka ya hivi karibuni, ukomo uliowekwa ni kikwazo kwa

nchi zinazoendelea hususani za Asia (India, Indonesia na Thailand) kununua chakula cha kutosha kutoka kwa wakulima wao.

Katika mkutano wa kumi wa Mawaziri (MC10) uliofanyika Nairobi, Kenya tarehe 15-19 Desemba, 2015, Mwaziri walirejea azimio lao walilolitoa kwenye mkutano wao wa tisa uliofanyika Bali, 2013 ambalo liliruhusu nchi masikini na nchi zinazoendelea kununua na kuhifadhi chakula wakati suluhisho la kudumu linaendelea kujadiliwa hadi kufikia mkutano wa kumi na moja (MC11) wa Mawaziri ambapo suluhisho la kudumu linatarajiwa kupatikana. Kwa mantiki hiyo, kwenye mkutano wa Nairobi, Mawaziri walitoa maamuzi ya nchi wanachama kuendelea na majadiliano kwa lengo la kuhakikisha kuwa suluhisho la kudumu linapatikana kwenye suala hili ifikapo mwaka 2017.

### *1.3* Ulegezaji wa Masharti ya Biashara ya Huduma kwa nchi Maskini *(LDCs Services Waiver)*

Ulegezaji wa masharti ya Biashara ya Huduma kwa nchi changa duniani *(LDCs Services Waiver)* ni moja ya masuala ya maendeleo ambayo yamefikia hatua nzuri ya majadiliano katika Shirika la Biashara la Dunia. Kwenye mkutano wa Bali, iliamuliwa kuwa nchi wanachama waanze kutekeleza mara moja hususani nchi zilizoendelea kutoa upendeleo maalum kwa watoa huduma kutoka nchi changa (LDCs). Ili kutekeleza hilo, nchi changa zilitakiwa kuainisha mahitaji yao *(identification of sectors of interests)* ambayo yataonyesha Sekta na njia za kutoa huduma hizo *(sectors and modes of supply)* ambazo wangependa nchi zilizoendelea ziwafungulie masoko yao ikiwa ni pamoja na kuondoa ama kulegeza masharti yanayowekwa na nchi zilizoendelea ambayo ni kikwazo kwa watoa huduma wetu kuingia katika masoko hayo. Baada ya utafiti uliofanywa nchini na Shirika la Canada ILEAP mwaka 2014 juu ya vikwazo vya ndani na nje vinavyozikabili Nchi changa (LDCs) katika sekta ya Biashara ya Huduma matokeo ya utafiti huo yalibainisha sekta za Kipaumbele tano zinazohitaji kuondolewa vikwazo ili ziweze kukua zaidi na kunufaika na fursa za upendeleo zilizotolewa na WTO, sekta hizo ni *Business, Transportation, Tourism and Travel Related Services, Finance*, *and Entertainment.* Aidha, Octoba mwaka 2015 shirika lingine la ICTSD lilijitolea kufanya utafiti kubaini vikwazo hususan vya ndani katika sekta ya Biashara ya Huduma kwa Nchi changa ikiwemo Tanzania na kubaini sekta za Kipaumbele nne zinazohitaji kuondolewa vikwazo ili ziweze kunufaika na fursa za upendeleo zilizotolewa na WTO, sekta hizo ni; *tourism and travel related services, transportation and*

*logistics services, cultural, sports and recreational services, and finance.* Baada ya utafiti huo, nchi yetu imeweka mpango wa muda mfupi na wa muda mrefu katika kuchochea ukuaji wa sekta hizo ambapo hatu ya kwanza ni kuweka katika tovuti ya Wizara sekta za Biashara ya Huduma ambazo mataifa wanachama wametoa kwa mataifa machaga (LDCs) pili ni kutatua vikwazo hivyo kwa kupitia upya sera na kanuni zenye mapungufu katika kuchochea ukuaji endelevu wa sekta hizo. Novemba 2015, nchi zilizotangaza sekta za upendeleo katika Biashara ya Huduma kwa nchi masikini zilifikia 19 ikijumuisha nchi za Canada; Australia; Norway; Korea; China; Hong Kong, China; Chinese Taipei; Singapore; New Zealand; Uswisi; Japan; Mexico; Turkey; Marekani; India; Chile; Iceland, Brazil na Umoja wa Ulaya (Œuropean Union). Sekta hizo ambazo zimetolewa kwetu na watanzania wanapaswa kuzichangamkia zimeambatishwa katika tovuti hii.

Aidha, kwa kuwa maamuzi ya ulegezaji masharti yalitolewa mwaka 2011 na kwa kuwa miaka minne imepita tangu maamuzi kutolewa, kwenye Mkutano wa Nairobi, Mawaziri waliamua kuongeza muda wa fursa ya upendeleo (*waiver)* hadi tarehe 31 Desemba, 2030.

### *1.4* Mfumo maalum wa kujikinga na ongezeko la uingizwaji wa bidhaa *(Special Safeguard Measure (SSM)*

Katika mkutano wa Nairobi, Mawaziri waliamua kuwa nchi masikini na zinazoendelea zina haki ya kutumia mfumo maalum wa kujihami kiuchumi dhidi ya ongezeko kubwa la uingizwaji wa bidhaa za kilimo kama mchele, sukari n.k toka nje ya nchi kama ilivyo kwenye aya ya saba *(paragraph 7)* ya Azimio la Mawaziri kwenye mkutano uliofanyika Hong Kong mwaka 2005.

Mfumo huu maalum wa kujihami (SSM) hutumiwa kwa kuongeza ushuru kwa kipindi maalum *(temporary period)* ili kuweza kukabiliana na ongezeko na uingizwaji wa bidhaa toka nje ili kusiadhiri uzalishaji wa ndani.

### 1.5 Utekelezaji wa makubaliano kwenye eneo la pamba *(Implementation of Cotton Commitments)*

Majadiliano kwenye eneo hili la pamba yamekuwa yakiongozwa na nchi za Benin, Burkina Faso, Chad na Mali (C4) na masuala makuu ambayo yamekuwa yakisisitizwa ni kuondolewa kwa misaada *(domestic support)* inayotelewa na nchi zilizoendelea kwa

wakulima wao wa pamba, upatikanaji wa masoko na uondolewaji wa ruzuku inayotolewa na nchi zilizoendelea kwenye uuzaji wa pamba.

Kwenye mkutano wa Mawaziri uliofanyika Nairobi, Desemba 2015, ilimualiwa kuwa pamba na bidhaa za pamba kutoka nchi masikini (LDCs) ziruhusiwe kuingia kwenye masoko ya nchi zilizoendelea, na kwenye nchi zinazoendelea zenye uwezo kufanya hivyo, bila ushuru na bila kikomo *(duty free quota free)* kuanzia Januari 2016. Kuhusu misaada/ruzuku inayotolewa kwa kuuza pamba nje, iliamuliwa kuwa nchi zilizoendelea zikataze mara majo utoaji wa ruzuku hiyo, na nchi zinazoendelea *(developing countries)* zitaondoa ruzuku hiyo hapo baadaye. Kuhusu utoaji wa misaada ya ndani *(domestic support)*, Mawaziri walibainisha kuwa mabadiliko kadhaa *(reforms)* yameshafanywa kwenye sekta pamba na wakasisitiza kuwa bado kuna haja ya kufanya mabadiliko zaidi.

### 1.6 Uasili wa Bidhaa *(Rules of Origin)*

Uasili wa Bidhaa ni eneo lingine muhimu sana kwa nchi maskini kwani pamoja na kupewa fursa mbali mbali za masoko ya upendeleo na nchi zilizoendelea, kama vigezo vya Uasili wa Bidhaa sio rahisi kutekelezeka vinaweza kuwa mojawapo ya vikwazo vya nchi maskini kuweza kutumia kikamilifu fursa mbali mbali zinazotokana na upendeleo wa masoko wanazopewa.

Kwenye eneo hili, kundi la LDC limekuwa lisisitiza urazinishaji wa Vigezo vya Uasili wa Bidhaa visivyo vya upendeleo *(Harmonization of non-Preferential rules of Origin)* ili ziweze kuyatumia kiukamilifu masoko ya upendeleo wanayopewa.

Katika mkutano wa Mawaziri uliofanyika Hong Kong mwaka 2005, Mawaziri walikubaliana kuhakikisha Vigezo vya Uasili wa Bidhaa kwa Masoko ya Upendeleo "preferential rules of origin" vinarahisishwa ili kuweshesha nchi za LDCs kutumia kikamilifu fursa ya masoko ya upendeleo. Pamoja na kuwepo makubaliano hayo nchi nyingi zinazotoa masoko ya upendeleo zilikuwa bado hazijatekeleza maagizo hayo na hivyo kuendelea kuwa vigumu kwa nchi za LDCs kutumia kikamilifu masoko hayo.

Suala hili lilipelekea mwaka 2007, kundi la nchi maskini ndani ya WTO kuwasilisha mapendekezo kutaka nchi zinazotoa masoko ya upendeleo kurazinisha *(harmonise)* Vigezo vya Uasili wa Bidhaa, suala ambalo lilipingwa vikali na nchi hizo kwa maelezo kuwa mpango wa kutoa masoko ya upendeleo ni wa kujitolea na hivyo hazitakiwi kuwajibishwa kimkataba au kwa kufungwa na maamuzi ya kisheria WTO.

Kupitia majadiliano yaliyochukuwa muda wastani wa maiaka mitano, mwaka 2013 katika mkutano wa tisa wa Mawaziri uliofanyika mjini Bali, Mawaziri walikubaliana kuwa na miongozo *(guidelines)* ya Vigezo vya Uasili wa Bidhaa kwa Masoko ya Upendeleo. Hata hivyo pamoja na kuwepo miongozo iliyokubaliwa kwenye mkutano wa Bali bado nchi wanachana zilikuwa bado hazijatekeleza maamuzi hayo kwa maana ya kurahisisha vigezo tajwa.

Kutokana na kuwepo kwa changamoto hiyo kundi la nchi za LDCs liliandaa mapendekezo yanayolenga kutekeleza makubaliano ya Bali ili kupunguza vikwazo vya kutumia masoko ya upendeleo vitokanavyo na vigezo vya uasili wa bidhaa. Mapendekezo hayo yaliwasilishwa kwenye mkutano wa 10 wa Mawaziri uliofanyika mjini Nairobi Desemba 2015 na Mawaziri walipitisha maamuzi ambayo pamoja na mambo mengine yalibainisha njia bora zaidi za kutambua uasili wa bidhaa kutoka nchi maskini ikiwa ni pamoja na wakati ambapo nchi maskini zinaweza kutumia malighafi kutoka nchi zingine na kuweza kuzalisha bidhaa *(cumulation)* ambazo zitaweza kuingia kwenye masoko ya upendeleo.

### *1.7* Uondoaji wa ruzuku za mauzo nje kwa mazao ya kilimo *(Export Competition)*

Nchi masikini na nchi zinazoendelea, kwa muda mrefu zimekuwa zikitoa hoja mbali mbali kuhusu madhara ya ruzuku zinazotolewa na nchi zilizoendelea kwenye mauzo ya bidhaa za kilimo nje ya nchi zao.

Kwenye mkutano wa Mawaziri wa Nairobi, suala hili lilijadiliwa na Mawaziri na maamuzi kadhaa yalifanyika. Moja ya maamuzi yaliyotolewa ni kwamba nchi zilizoendelea *(developed countries)* ziondoe ruzuku hizo mara moja na nchi zinazoendelea (developing) zitaondoa ruzuku hizo ifikapo mwaka 2018. Nchi zinazoendelea zitakuwa na upendeleo *(flexibility)* kwenye gharama za masoko na usafirishaji wa bidhaa za Kilimo hadi mwaka 2023 na nchi masikini zitakuwa na muda wa ziada zaidi wa kuondoa ruzuku hizo.

## 2.0 MAENEO MENGINE YA MAJADILIANO

### *2.1* Masoko kwa bidhaa zisizo za Kilimo *(Non Agriculture Market Access - NAMA)*

Kwenye eneo hili nchi za LDC zinataka upendeleo maalum wa kutopunguza ushuru wa bidhaa pamoja na kuwa na mwanya wa kisera *(Policy Space)* kwa ajili ya maendeleo ya viwanda. Maeneo maalum yaliyowekewa mkazo ni pamoja na:

i) Upatikanaji wa masoko ya uhakika *(Substantial improvement in market access).*

ii) Kushughulikia vikwazo vya biashara visivyo vya kiushuru (NTBs) kutokana na ukweli kwamba vimekuwa vikikwamisha biashara ya nchi masikini na zinazoendelea kwa kiwango kikubwa. NTBs zimekuwa zikitumiwa na nchi zilizoendelea kama mbadala wa ushuru katika kuzuia biashara. Nchi zilizoendelea zinataka suluhu itafutwe kwanza kwenye suala la ushuru/kodi na suala la NTBs lifanyiwe kazi baadaye. Nchi maskini na zinazoendelea zinataka masuala yote mawili yaende kwa pamoja kwani yana athari sawa ya kuzuia bidhaa kuingia kwenye soko la nchi zilizoendelea.

iii) Kuendelea kudumisha upendeleo maalum kwa nchi zenye uchumi mdogo *(Small and Vulnerabl Economie-SVE)* na nchi Maskini (LDCs). Tangu kuanzishwa kwa majadiliano ya Duru la Doha ilikubaliwa kuwa SVEs na LDCs hazipaswi kupunguza ushuru *(no tariff cuts).*

### 1.3. Uvuvi (Fisheries)

Uvuvi kwa nchi maskini ni eneo ambalo linachangia kwenye upatikanaji wa mapato, ajira na chakula kwa watu wengi na hivyo ni eneo ambalo kama likiendelezwa linaweza kuwa na mchango mkubwa sana kwenye maendeleo ya nchi ikiwa ni pamoja na kupunguza umasikini. Kwa maantiki hii, nchi za LDCs zimeweka wazi kwamba majadiliano ni lazima yalenge katika; -

*i)* Kuimarisha mfumo wa upashanaji habari na uwazi *(Enhance transparency mechanism).*

*ii)* Kuondoa ruzuku zote zinazotolewa kwenye uvuvi na kusababisha biashara ya samaki kutokuwa ya haki na usawa *(discipline all type of subsidies going in fishery sector which adversely affect fair trading of fish and fish products).*